# CLASS 6 MID TERM 3 DECEMBER 2021
# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Ilianza__1__mzaha tu. Mawingu kidogo kidogo__2__ kujikusanya. Mara upepo mkali ukaanza __3__kutoka upande wa mashariki na kupukusa majani ya miti.__4__mvua kubwa ikaanza kumwagika ikifuatwa na mngurumo wa__5__. Kila mtu akawa ni__6__niponye akitafuta pa kujisitiri.

__7__wa kale walisema dalili ya mvua ni mawingu. Lakini hii__8__hivyo. Hakukuwa na dalili __9__ya mvua. Mchana__10__ jua liliwaka kwa hasira na kuwafanya waja kulaani. Hivyo__11__binadamu walivyo. Hawatosheki na__12__. Hawakosi kunung'unika, kuwe baridi, jua__13__mvua. Naye Mola akawasikia na kujibu dua__14__ilipotimu wakati wa magharibi upepo, mvua na radi zikasikika. Ikawa dalili ya mvua ni mawingu. __15__ikawa sasa ni yakunya haina wingu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **A.** kama | **B.** na | **C.** bila | **D.** pamoja |
| 2. | **A.** ikaanza | **B.** likaanza | **C.** yakaanza | **D.** zikaanza |
| 3. | **A.** kunguruma | **B.** kuvuma | **C.** kupiga | **D.** kuzuka |
| 4. | **A.** Gafla | **B.** Hafla | **C.** Ngafla | **D.** Ghafla |
| 5. | **A.** radhi | **B.** radi | **C.** randi | **D.** rati |
| 6. | **A.** mguu | **B.** mkuu | **C.** Mungu | **D.** guu |
| 7. | **A.** Waganga | **B.** Washenga | **C.** Wahenga | **D.** Malenga |
| 8. | **A.** ilikuwa | **B.** itakuwa | **C.** haiwi | **D.** haikuwa |
| 9. | **A.** lolote | **B.** zozote | **C.** chochote | **D.** yoyote |
| 10. | **A.** kote | **B.** wote | **C.** yote | **D.** lote |
| 11. | **A.** ndiyo | **B.** ndio | **C.** ndivyo | **D.** ndipo |
| 12. | **A.** chochote | **B.** yeyote | **C.** yoyote | **D.** wowote |
| 13. | **A.** pia | **B.** wala | **C.** na | **D.** ila |
| 14. | **A.** wao | **B.** lao | **C.** chao | **D.** yao |
| 15. | **A.** Bali | **B.** Wala | **C.** Na | **D.** Tena |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Wingi wa neno mwanajeshi ni wanajeshi nao wingi wa neno polisi ni
A. wapolisi. B. wanapolisi.
C. polisi. D. mapolisi.

**17.** Kamilisha sentensi kwa kivumishi sahihi
*Fisi amemla ng'ombe ________ akammaliza.*
A. lote B. yote
C. wote D. chote

**18.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo
Wembe wowote utafaa kukatia.
A. Wembe zozote zitafaa kukatia.
B. Nyembe zozote zitafaa kukatia.
C. Mawembe yoyote yatafaa kukatia.
D. Vijembe vyovyote vitafaa kukatia.

**19.** Akifisha kwa usahihi sentensi ifuatayo:
*Nimemaliza kazi mwanafunzi alisema.*
A. Nimemaliza kazi, "mwanafunzi alisema."
B. "Nimemaliza kazi, mwanafunzi alisema."
C. "Nimemaliza kazi." mwanafunzi alisema.
D. "Nimemaliza kazi," mwanafunzi alisema.

**20.** Ni sentensi ipi imetumia kiulizi -ngapi kwa usahihi?
A. Wamepanda miti mingapi?
B. Ni vifaru vingapi vimeuawa?
C. Umekula machungwa ngapi?
D. Wameunda mashine mangapi?

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

21. Tambua kielezi katika sentensi ifuatayo
Mwashi alijenga nyumba vizuri.
A. alijenga B. vizuri
C. mwashi D. nyumba

22. Kamilisha sentensi kwa kivumishi cha idadi sahihi
Kulikuwa na mwanafunzi ________ darasani.
A. watisa B. wasaba
C. wasita D .wanane

23. Andika umoja wa sentensi ifuatayo
Mihindi imeangushwa na upepo.
A. Mhindi umeangushwa na upepo.
B. Mhindi ameangushwa na upepo.
C. Hindi imeangushwa na upepo.
D. Hindi limeangushwa na upepo.

24. Chagua neno lililotofauti na mengine
A. Jengo. B. Mjenzi.
B. Jenga. D. Ujenzi.

25. Ni kivumishi gani kisichochukua kiambishi?
A. Zuri. B. Karimu. C. Kali. D. Baya.

26. Ni sentensi ipi imetumia 'karibu' kama kihusishi?
A. Alijikwaa; karibu aanguke.
B. Mvua I karibu kunyesha.
C. Kwao ni karibu na kwetu.
D. Karibu tule chakula.

27. Ni gani kati ya hizi si kiungo cha kupikia?
A. Udi. B. Dania. C. Iliki. D. Limau.

28. Kutokana na mchai tunapata majani chai; je, kutokana na mbuni tunapata nini?
A. Korosho. B. Mchele.
C. Ufuta. D. Kahawa.

29. Unapoambiwa karibu utajibu vipi?
A. Ninashukuru B. Starehe.
C. Asante. D. Nimeshiba.

30. Kisawe cha ukuta ni __________
A. daftari. B. nguzo.
C. kiambaza. D. dari.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kufaulu kwa mwanafunzi katika masomo kunategemea sana ushirikiano wa watu watatu: mwalimu, mzazi na mwanafunzi mwenyewe. Ushirikiano huu aghalabu hulinganishwa na mafiga, yale mawe matatu, ambayo bila mojawapo chakula hakiwezi kikapikika. Chambilecho wahenga umoja ni nguvu utengano ni udhaifu katika ushirikiano kila mmoja ana sehemu ama jukumu lake. Lakini jukumu kubwa zaidi ni la mwanafunzi.

Watu wengi, na hasa wanafunzi na wazazi, hudhani kuwa jukumu la kumfanya mwanafunzi afaulu masomoni lote ni la mwalimu. Dhana hii si sahihi. Hata ingawa mwalimu ni kiungo na mshiriki muhimu katika kumwelekeza, kumrekebisha na kumwelimisha mwanafunzi, hana uwezo wa kumfanya afaulu. Uwezo huu umo ndani ya mwanafunzi mwenyewe. Takribani asilimia sabini ya mchango wa ufanisi masomoni wafaa kutoka kwa mwanafunzi. Hii haimpi mwalimu kibali cha kuzembea; la hasha! Lakini hata mwalimu akiweka juhudi zake zote; na atumie ujuzi na maarifa yake yote, atamsaidia vipi mwanafunzi kufaulu iwapo yeye mwenyewe hatakuwa na ari na nia yakufanya hivyo? Palipo na nia pana njia. Wakasema wahenga. Bila nia, yote ni bure. Ni sawa na kumpigia mbuzi gitaa waambavyo wenye hekima wengine.

Baadhi ya wazazi nao hukwepa majukumu yao. Wanapomfikisha mwanafunzi shuleni na kumkabidhi mwalimu huwa ni 'kwaheri ya kuonana'. Yanayoendelea kati ya mwanafunzi na mwalimu huwa hayawahusu ndewe wala sikio. Mambo yanapoenda mrama lawama zote huelekezewa mwalimu. Haifai kuwa hivyo; hasa iwapo mwalimu ametimiza wajibu wake. Kila mtu na atekeleze wajibu wake ili kusiwe na sababu ya kulaumiana. Lakini itakuwaje iwapo kila mtu ametimiza wajibu wake kisha mambo yaende mrama?

Yawezekana mwalimu, mzazi na mwanafunzi wakashirikiana vyema na bado matokeo bora yakakosekana. Ni lazima tutafute sababu ya mwanafunzi kutofaulu kabla ya kumlaumu. Ni lazima ifahamike kuwa kutofaulu katika mtihani mara nyingine si ujinga. Kunaweza kusababishwa na hali ya kiafya, ugumu wa maisha (hali ya kiuchumi) ama sababu za kimaumbile. Sababu za kiafya na kiuchumi wakati mwingine zinaweza zikarekebishika na mwanafunzi akaendelea vyema kimasomo. Lakini sababu za kimaumbile si rahisi kurekebishika. Hivyo basi mwalimu hana budi kutafuta na kutambua vipawa vingine alivyo navyo mwanafunzi mbali na masomo ya darasani. Mwalimu anapaswa kumfahamisha mzazi ili waweze kushirikiana katika kukuza vipawa vya mwanafunzi. Hii inaambatana na mfumo mpya wa elimu yaani CBC. Bila shaka mwanafunzi asipofurahi kwa njia moja ni lazima atafaulu kwa njia nyingine.

31. Kufaulu kwa mwanafunzi kunategemea sana ushirikiano wa watu watatu. Ni nani hakutajwa kati ya hawa?
A. Mwalimu.
B. Mzazi.
C. Mwanafunzi.
D. Mhazili.

32. Kati ya watu hao watatu, jukumu kubwa zaidi ni la nani?
A. Mwanafunzi. B. Mzazi.
C. Wote. D. Mwalimu.

33. Watu wengi hudhani kuwa jukumu la kumfanya mwanafunzi afaulu lote ni la
A. mwalimu mkuu.
B. mwanafunzi.
C. mwalimu.
D. mzazi.

34. Mwalimu ni kiungo na mshiriki muhimu katika kumtendea mwanafunzi yafuatayo isipokuwa
A. kumwelekeza.
B. kumrekebisha.
C. kumwelimisha.
D. kumpotosha.

35. Hata mwalimu akiweka juhudi zake zote, mwanafunzi hawezi kufaulu asipokuwa na
A. ari na nia.
B. uzembe na nia.
C. ari na njia.
D. nia na njia.

36. Mambo yanapoenda mrama lawama zote huelekezwa
A. mwanafunzi. B. mwalimu.
C. mwalimu mkuu. D. mazazi.

37. Kulingana na aya nne kutofaulu katika mtihani mara nyingine hakusababishwi na
A. hali ya maisha.
B. ujinga.
C. hali ya kiafya.
D. sababu za kimaumbile.

38. Ni sababu gani ambazo wakati mwingine zinaweza kurekebishwa na mwanafunzi akaendelea vyema kimasomo?
A. Kiafya na kimaumbile.
B. Kiuchumi na kimaumbile.
C. Kiafya na kiuchumi.
D. Kiuchumi na kiakili.

39. Mbali na masomo ya darasani, mwalimu anapaswa kutafuta na kutambua
A. hali ya kiafya ya mwanafunzi.
B. hali ya kiuchumi ya mwanafunzi.
C. hali ya kimaumbile ya mwanafunzi.
D. vipawa alivyo navyo mwanafunzi.

40. Ni kichwa gani kinachofaa kifungu hiki?
A. Kufaulu kwa mwanafunzi.
B. Kazi ya mwalimu.
C. Jukumu la mzazi.
D. Jukumu la mwanafunzi.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Safari yangu ya kwenda Tharaka-nithi ilianza asubuhi na mapema. Hii ni kwa sababu nilitaka niende na nirudi Nairobi kabla ya saa za kafyu. Matatu niliyoabiri ilienda kwa mwendo wa kadiri; si kasi sana na si polepole sana. Hivyo tukawasili Tharaka-nithi salama salmini.

Kutoka Nairobi kwenda Tharaka-nithi ni sharti upite kaunti tatu. Kaunti hizi ni Murang'a, Kirinyaga na Embu. Njiani nilijionea mandhari ya kuvutia-milima, mabonde, mito na misitu. Vilevile nilijionea nchi tambarare ya Mwea kunakokuzwa mpunga. Nchi ilionekana kama iliyofunikwa kwa zulia la kijani kibichi lililotandazwa hadi upeo wa macho.

Nilikuwa nimeenda kuzuru shule ya upili ya Kangema anayosomea mwanangu Ollopa. Nilikuwa nikiitikia mwito kutoka kwa mwalimu ulionitaka nifike kwa haraka; likataliwalo ni neno uliloitiwa. Naam utalikataa uliloitiwa ikiwa tu ni baya au halifai.

Nilikuwa nimepata ujumbe mfupi kupitia kwa rununu. Mwalimu wa darasa alikuwa ametatizika kuhusu maendeleo ya Ollopa kimasomo na hivyo akanitaka nifike shuleni ili tuweze kujadiliana. Mwalimu alinifahamisha kuwa Ollopa alikuwa amezembea katika kudurusu na kukamilisha kazi za walimu; jambo ambalo lilichangia matokeo mabaya katika mitihani. Lililokuwa likitia wasiwasi zaidi ni kuwa mwake ambao angefuata, Ollopa alikuwa afanye mtihani wake wa mwisho wa kidato cha nne. Mwalimu Muchiri alionyesha moyo wa kujali sana.

Baada ya mazungumzo yetu na mwalimu alimwita Ollopa ofisini. Alimhoji na kumshitaki mbele yangu.

Jambo la kutia moyo ni kuwa Ollopa hakukanusha mashtaka. Aliyakiri na kuomba msamaha kwa mwalimu wake na kwangu mzazi wake. Aliahidi kuwa hangerudia tena makosa hayo na kuwa angetia bidii masomoni. Ili kutuhakikishia kuwa atayazingatia aliyoyasema, mwalimu alimtaka aandike barua. Alifanya hivyo.

Yapata mwendo wa saa tisa alasiri, nilifunga safari ya kurudi Nairobi; huku nikiwa na matumaini kuwa yote yatakuwa sawa. Safari ya kurudi haikuwa shwari kama ya kwenda. Jamu katika barabara kuu ya Thika iligeuka jinamizi. Ikasababisha Mlolongo mkubwa wa magari. Polisi wa trafiki walifanya kazi ya ziada kujaribu kuifungua. Lakini baada ya muda mfupi madereva watundu walifungiana wakijaribu kupita wenzao. Hata hivyo tuliweza kufika Nairobi salama kabla ya saa za kafyu.

Ushirikiano wangu na mwalimu ulizaa matunda; kwani mwanangu Ollopa alibadili tabia na mwenendo wake. Alitii na kushirikiana na walimu wake vyema. Alijitahidi katika kudurusu na kufanya kazi zote alizopewa na walimu wake. Walimu walimpenda na kumsaidia wakati wowote alipohitaji msaada wao. Mwamko wake mpya, nidhamu na bidii vilimwezesha kufaulu katika mtihani wake wa mwisho wa kidato cha nne. Kweli kinga na kinga ndipo moto.............

---

**41.** Kwa nini mwandishi alianza safari asubuhi na mapema?
A. Alitaka afike mapema.
B. Alikuwa anaenda mbali.
C. Alitaka arudi Nairobi kabla ya saa za kafyu.
D. Alitaka arudi Nairobi aripoti kazini.

**42.** Matatu aliyoabiri ilienda kwa mwendo wa
A. kadiri.
B. kasi sana.
C. polepole sana.
D. asteaste.

**43.** Ni kaunti gani mwandishi hakupitia alipokuwa akienda Tharaka-nithi?
A. Murang'a.
B. Meru.
C. Kirinyaga.
D. Embu.

**44.** Unadhani zulia la kijani kibichi lililokuwa limetandazwa hadi upeo lilikuwa ni nini?
A. Mashamba ya majani chai.
B. Mashamba ya kahawa.
C. Mashamba ya maua.
D. Mashamba ya mpunga.

**45.** Mwandishi alienda Tharaka-nithi kufanya nini?
A. Kujionea mandhari ya kuvutia.
B. Kuzuru shule aliyosomea mwanawe.
C. Kununua mchele.
D. Kujionea zulia la kijani kibichi.

**46.** Kulingana na aya nne, Ollopa alikuwa kidato cha ngapi?
A. Cha nne.
B. Cha kwanza.
C. Cha tatu.
D. Cha pili.

**47.** Ni nini kilichotia wasiwasi zaidi?
A. Kuzembea kwa Ollopa katika kudurusu.
B. Matokeo mabaya katika mtihani.
C. Maendeleo ya Ollopa kimasomo.
D. Ollopa alikuwa afanye mtihani wake wa mwisho mwaka ambao ungefuata.

**48.** Baada ya Ollopa kushtakiwa mbele ya mzazi wake, mambo yafuatayo yalikuwa ya kutia moyo isipokuwa
A. alimpuuza mwalimu na mzazi wake.
B. aliyakiri makosa yake.
C. aliomba msamaha.
D. aliahidi kutorudia makosa na kutia bidii.

**49.** Safari ya kurudi Nairobi haikuwa shwari. Ni nini kilichosababisha hilo?
A. Jinamizi katika barabara kuu ya Thika.
B. Jamu katika barabara kuu ya Thika.
C. Polisi wa trafiki.
D. Ajali barabarani.

**50.** **Kamilisha methali:**
*Kinga na kinga ndipo moto*
A. uzimapo B. upoapo
C. uwakapo D. ochomapo